Vitu Hatari

Mfululizo wa Vitabu vya Kuunganishwa kwa Damu Kitabu cha 3

Lugha: Kiswahili

Amy Blankenship, RK Melton

Table of Contents

Sura ya 1
Sura ya 2
Sura ya 3
Sura ya 4
Sura ya 5
Sura ya 6
Sura ya 7
Sura ya 8
Sura ya 9
Sura ya 10
Sura ya 11
Sura ya 12
Sura ya 13
Sura ya 14
Sura ya 15
Sura ya 16

Vitu Hatari
Mfululizo wa Vitabu vya Kuunganishwa kwa Damu Kitabu cha 3
Mfululiza wa Vitabu vya Kufungwa kwa Damu

Amy Blankenship, RK Melton
Translator: Zawadi Adhiambo

Hakimiliki © 2012 Amy Blankenship
Toleo la Pili Kimechapishwa na TekTime
Haki zote zimehifadhiwa.

Sura ya 1

Envy alishughulika kote chumbani mwake akipakia vitu vyake ndani ya sanduku lake leusi la ngozi. Alisita na kumkazia macho kaka yake alipotambua kuwa alikuwa akivitoa vitu vyake kila wakati alipogeuka kuchukua vyengine. Alikuwa akimfokea tangu aliporudi nyumbani na alikuwa akianza kukasirishwa naye.

“Wacha,” Envy alifoka akizitoa nguo kadha mkononi mwake na kuzirudisha ndani ya sanduku. Alizirusha nywele zake nyekundu ndefu begani mwake na kumkazia jicho la kumuonya.

“Lakini kuhama? Umemjua tu kwa muda gani… juma moja? Unahakika kuwa hili ndilo unalotaka kufanya?” Chad alirudia kama mantra.

“Jibu bado ni lile lile Chad,” Envy alimueleza kwa sauti imara, akijiuliza kuwa itambidi aliseme mara ngapi kabla ya kumsikiza. Alimkazia macho na, kumfanya kama mtoto asiye elewa haraka, aliyasema maneno kwa taratibu sana, “ninataka kuishi na Devon, na hilo ndilo ninaloenda kufanya.”

“Unaweza kuwa vipi na hakika kuwa ndani ya juma au mwezi mmoja kutoka sasa, hatampata msichana mwengine na kukuwacha?” Chad alidai kwa kukata tamaa.

“Hata wahi.” Aliendelea kupakia, akijaribu kuizuia hisia ya kuwa alikuwa akimtenga kaka yake. Alikuwa mwanamume aliyekomaa, na hata afisa wa polisi.

“Hulijui hilo kwa hakika. Nina maanisha, anacheza densi nusu uchi ndani ya kilabu kile kila usiku na wewe utabaki nyuma ya baa ukiwapa pombe wapotovu.” Chad alisema akiwa tayari kuzivuta nywele zake. Kile alichokuwa akitaka kukifanya ni kumfokea kwa kujihusisha na jambo hatari namna hio… na mtu hatari hivyo.

Envy alisita kuzipakia nguo na kumuangalia kaka yake wa pekee aliyempenda kwa dhati lakini akiwa tayari kunmyonga. “Moja, ninajua kwa hakika. Pili, huenda akawa nusu uchi, lakin anaonekana mzuri sana akiwa hivyo. Tatu, nitacheza densi naye pale kwenye kizimba. Na nne,” alisongea karibu kanakwamba anatoa siri chafi, “kwa hakika unahitaji kuwa na mwanamke.”

Chad alimkazia mdogo wake mache, “si hitaji kufanya mapenzi.” Alinguruma wakati Envy alipomuinulia nyusi.

“Ndio, unahitaji.” Alifungua droo na kuchukua nguo kadha za ndani.

“Hapana, si hitaji.” Chad alilifunga sanduku kabla ya kuzionge kwenye sanduku aliyotumai kuwa lilikuwa la siku chache tu.

“Ndio unahitaji.” Envy alizitingisha nguo zile za ndani usoni mwake kana kwamaba kumuonyesha hoja yenyewe.

“Hapana si hitaji.” Alizitoa mkononi mwake.

“Hapana huhitaji.” Envy aliyakunja macho yake kwa hasira.

“Ndio ninahitaji.” Chad alisita kisha akaipiga ngumi iliyokuwa imeshikilia zile nguo za ndani juu ya hewa. “UPUZI!”

Devon alikuwa kule sebuleni akiwa ameuegemea ukuta na kuuweka mguu mmoja juu ya mwengine na mikono yake kwenye mifuko ya suruali yake…akijaribu kujizuia asicheke. Ubishi wao ulimkumbusha sana kuhusu uhusiano wake na ndugu zake wapendwa.

Aliona kuwa Chad alimjali sana Envy, na kwa sababu ya hilo, hangesimama kati yao. Chad alikuwa akilifanya alilokuwa analifanya vyema… alikuwa kaka ya msichana mmoja mwenye nywele nyekundu aliyekuwa na moto mwingi. La, hatawazuia, lakini angelipa pesa nzuri kuangalia tu.

Devon alicheka kwa sauti kisha akajaribu kukificha na kikohozi cha uongo. Mtu alibisha mlangoni na aliyakunja macho yake ya barafu ya samawati akijiuliza ni nani aliyekuwa akiwatembelea ndugu hawa asubuhi mapema hivi.

“Devon, unaweza kunifungulia mlango?” Chad alisema.

“Sawa,” Devon alijibu na kujisukuma kutoka ukutani kabla ya kuelekea kwenye kiingilio. Akiufungua mlango, hangejizuia kucheka kwa ule muangalio wa mshangao uliokuwa usoni mwa Trevor. “Hujambo Trevor, hatujaonana muda mrefu.”

Kama alivyoahidi, Trevor alikuwa amekuja kuongea na Chad kuhusu alichokiona pale kanisani. Jambo la mwisho alilotarajia ni Devon Santos kuufungua mlango. Asiweze kuzizuia hisia zake, Trevor mara ile ile aliuinua mkono na kumpiga yule chui kwenye pua lake… kwa nguvu.

Devon alikunguwaa na kurudi nyuma hatua kadha kisha kuifuta damu kutoka kwenye pua lake. Aliiangalia kisha kumuangalia tena Trevor, na kutolea meno. Kabla ya Trevor kusonga, Devon aliminyana naye hadi nje ya mlango hadi nje ya nyumba.

Nguo ziliraruka na kuanguka wakati wawili hawa walipojibadili kwa maumbo yao ya kinyama. Devon alimzunguka yule Dubu na kumrukia kwa sauti kubwa ya chui. Trevor alinguruma na kuinuka kwenye miguu yake ya nyuma wakati akijaribu kumkamata yule chui aliyejibandika kwenye mgongo wake.

Ndani, Chad na Envy waliusikia mngurumo wa Devon na kukimbia pale nyumbani hadi mlango wa mbele. Walisimama walipomuona Devon akipigana na Dubu mkubwa pale mbele ya nyumba yao. Yule afisa wa polisi alishukuru kuwa hawaishi mahali panapoonekana kwa urahisi na majirani wao.

Chad aliizima swichi ya akili yake mara moja, na kuzizima hisia zake zote. Kilikuwa kitu kilicho bonyeka ndani yake ambacho kilimfanya awe mtulivu kabisa… hata kati ya vita vya bunduki. Akikifikia kifuniko cha bunduki kwenye paja lake la kulia, Chad aliitoa bunduki na kupiga juu ya hewa mara moja akijaribu kuwafanya wamuangalie. Alikunja uso wakati hio hata haiku wa shtua na akapata ngumi kwenye mkono wake wa kushoto.

“Mwambie mtu wakati unataka kufyetua kitu hicho!” Envy alisema wakati akishika mkono juu ya sikio lake la kulia na kujikunja kwa ile sauti kubwa iliyokuwa ikipiga sikioni mwake.

Zakaria alitoka nje ya gari lake na kuvuta pumzi kwa nguvu na kuwaangalia wale watoto wawili waliokuwa wakipigana. Kwa mara nyengine, akili tulivu itabidi iingilie kati. Akicheka mzaha wake mwenyewe kwa sababu hakuna anayeweza kulitumia neno akili tulivu kumueleza. Akiunua mkono wake mbele yake, alirusha wimbi la joto kuwaelekea wabadili viungo hao wawili, na kuwafanya waruke nyuma wakati mkondo mmoja wa moto uliporuka nje ya ile nyumba na kuwa tenganisha.

“Ikiwa nyinyi wawili hamtaki manyoya yenu yachomwe, basi itabidi mugeuke kuwa wanadamu tena na kujifanya kanakwamba muna akili timamu,” Zakaria alionya wakati mwali mwengine wa moto ulipoanza ulipoanza kukua kutoka kwenye mkono wake uliokuwa wazi. “Je, mtafanya kama watu wazima au watoto, kwa sababu haibadilishi chochote kwangu?” aliwapa tabasamu baridi wakati ule mwali ulipoendelea kukua juu zaidi na kuegemea kuelekea walengwa wake.

Wakijua kuwa Zakaria atalifanya, Trevor alijibadili tena kuwa mwanadamu na kukaza macho kuupita ule moto na kumuelekea mpinzani wake. Kumuangalia tu yule mwanamume aliyempokonya Envy kulifanya

msukumo wa damu kupanda juu sana ilimbidi kuwa makini sana ilikuiweka hali yake ya uwanadamu.

Devon alijibadili lakini akabaki katika hali ya vita, asimuamini Trevor. Alikengeushwa kwa muda alipoisikia sauti ya juu ya Chad “Mungu wangu” na kwa haraka akawaangalia wale ndugu. Alipomuona Envy akimuangalia Trevor… aliyekuwa angali uchi macho wazi, Devon alinguruma kwa undani akitaka umakini wa Envy urudi unapofaa… kwake

Envy aliusugua uso wake sasa wakati wanaume wote wawili walipokuwa uchi, kwa bahati nzuri wakiwa na vidonda vidogo. Devon alimuonyesha jinsi wabadili viungo wanavyoweza kupona kwa haraka kwa hiyo alijua kuwa mambo hayakuwa mabaya kama yalivyoonekana. Macho yake yalimuelekea Trevor, bado akiwa ameshtuka kuwa alikuwa akitoka nje na dubu kwa muda mrefu bila ya kulijua.

Trevor alicheka akifurahia kuwa mngurumo wa Devon ulikuwa sauti ya wivu safi…chui yule alistahili kuhisi hivyo.

Chad alipesa macho akijiuliza ni nani aliyempa aside. Kwa kawaida yeye huwa mtulivu katika hali mbaya, alivuta pumzi kwa ndani kisha akatoka mbali na mlango na kusimama kwa urefu wake wote. “Hii ni nyumba yangu, kwa hiyo mta fuata sheria zangu. Envy anakaa hapa nami, na kila mmoja ambaye si mwanadamu anatoka.” Alijaribu kuufunga mlango lakini Envy alimzuia.

“Siendi bila mwenzangu,” Devon alinguruma akijaribu kuitikisa ile athari ya mwangwi aliyokuwa akipata. Nani alijua kuwa Trevor alikuwa na nguvu kiasi hicho? Ufahamu huo hauku kaa vizuri ndani yake.

“Vaeni nguo zenu,” Envy alikunja uso kisha akarudisha macho yaliyokuwa na maswali upande wa Zakaria. Ilionekana kana kwamba yeye na Trevor wangekuwa ndugu, rangi zao zili fanana. Tofauti moja tu ya kweli ilikuwa kuwa Zakaria alikuwa na nywele fupi na alikuwa mrefu kidogo. “Sawa, ninajua wao ni nini… lakini wewe ni nini?”

Zakaria aliinama kiungwana, “Unaweza tu kuniita mlinzi,” alijinyoosha na kumuangalia Trevor. “Kwani hukumwambia chochote?”

“Hapana, hakuniambia,” Envy alimuangalia Trevor kwa macho mabaya kama alivyo stahili kisha akamgeukia Zakaria. “Mlinzi? Hiyo inamaanisha nini? Na je, wewe na Trevor ni ndugu?” Hangejizuia kuuliza.

“Inamaanisha kuwa tunalinda pande zote mbili kutoka kwa kila mmoja,” Trevor alijibu kisha akaongezea, “Na hapa. Kama familia zilivyo, sina yeyote.”

“Oh, sasa ghafla umejaa habari,” Envy alinung’unika.

“Nilijaribu kukwambia,” Trevor alimkumbusha wakati akiivuta juu suruali aliyorushiwa na Zakariya. “Sio makosa yangu kuwa hukusikiza.”

Midomo ya Envy ilifunguka kumtoa makosa lakini akasita… akikumbuka kwa hatia usiku ule wa mwisho alipomuona Trevor. Alimwambia kuwa alikuwa akifanya kazi na C.I.A. lakini hakumuamini. Hata alimpiga shoti kwa kufikiria kuwa alikuwa mjinga kiasi cha kuamini uongo kama huo. Lakini tena, alitarajia amuamini vipi wakati alipokuwa nje akicheza densi na wanawake wengine?

Upande wa chini wa jambo hilo ilikuwa… alimuambia kuwa ilikuwa ni kwa sababu ya kuweka siri kwa ajili ya kazi yake. Anvy alikunja uso wakati kichwa kilipoanza kumuuma na akaamua kuwa Trevor alikuwa mshenzi kuliko alivyofikiria kwa sababu ya kumfanya ayafikirie haya.

Chad alimuangalia yule chui kabla ya kuelekea ndani. Alirudi baada ya sekunde chache baadaye na suruali akamrushia Devon.

“Hatuhitaji msaada wake,” Devon alisema akiifunga suruali kisha kutembea hadi alipokuwa Envy na kumwekea mkono wa wivu kiunoni.

“Kweli? Nilimuokoa mdogo wako wa kike wakati ulikuwa na shughuli nyingi kumuiba mpenzi wangu,” kabla ya kuyarudisha macho yake kwa Envy.

Envy aliyainua macho yake na kuyakaza juu ya macho ya samawati ya Trevor. Bado angaliweza kuuona uchungu ndani yake na ikafanya moyo wake kuvuta kwa njia isiyofaa. Kwa kweli hakumchukia hata kidogo. Ukweli ni kuwa bado alimpenda Trevor… lakini sio kama vile alivyompenda Devon. Midomo yake ilifunguka akijaribu kueleza, lakini Devon akamkatiza.

“Kwanini ulikuja hapa? Je, ulitufuata?” Devon aliuliza, asipende jinsi Trevor alikuwa akimfanya Envy asijihisi sawia. Envy alikuwa tayari amefanya uamuzi wake na Trevor alihitaji kukubaliana na ukweli huo mdogo kabla umtie kwenye shida.

“Kwa kweli, alikuja hapa kuniona,” Chad alisema kwa utulivu kadri alivyoweza. Akimgeukia mdogo wake wa kike, aliuchukua mkono wake na kumvuta taratibu akimuangalia Devon. “Tafadhali, tuna dakika moja farahga.”

Mara tu Devon alipomuachilia, Chad alimvuta ndani ya mlango na kuufunga. Ilimbidi ajizuie kuifunga kwa kufuli. Kando na hilo, baada ya yale aliyoyaona hapo nje ya nyumba, kifuli hakingeweza kuzuia chochote.

“Unahakika kuwa hautakaa hapa kwa usiku mmoja tu zaidi hapa? Kwa ajili ya amani yangu?” aliomba, hata kama alijua kuwa amepoteza usukani wa maisha yake hapo awali.

Envy alimkumbatia kaka yake, kisha akachukua hatua nyuma kumuangalia, “siwezi. “Ulikiona kilichofanyika pale kanisani usiku wa leo. Kila mmoja ametawanyika, kwa hiyo Warren anajaribu kuitisha mkutano jambo la kwanza asubuhi.”

Aliangalia nyuma mlangoni wakati wazo lengine lilipomjia. “Kandona hilo, kukaa nao huenda ikawa mahali salama zaidi kuwa wakati huu. Nitakupigia simu nikwambie ni wakati gani utakuja kwenye mkutano na ikiwa utakuwa kwenye kilabu cha Densi ya Mwezi au Mwanga wa Usiku. Nakuomba uwalete Trevor na kijana wa moto kwenye mkutano, kwa sababu ikiwa niliyo yasikia hapo nje ni ukweli… tutahitaji msaada wote tutakaoweza kupata.”

“Wafyonza damu?” Chad aliuliza akirudi katika hali ya polisi tena hata akisugua nyuma ya shingo yake mahali ambapo nywele ndogo zilipoamua kusimama kwa msisimko.

Envy aliitikia, akakunja uso, kisha akatikisa kichwa, “Wafyonza damu ndio, lakini kuna pepo aliyeachiliwa na…”

Chad alimfikia na kuushika mkono wake, “Pepo? Hakuna aliyesema chochote kuhusu mapepo!”

Envy alivuta pumzi kisha akaitikia, akitumaini kuwa kile alichokuwa akitaka kulisema kitamfanya ahisi vizuri, “Ndio, pepo. Habari njema ni kuwa tuna malaika wawili upande wetu.” Alimpa tabasamu hafifu akitumai kuwa hata zimia.

“Malaika?” Chad alimuachilia na kuinama kwa nguvu dhidi ya ukuta, “Mungu Mzuri.”

“Hasa,” Envy aliitikia akimuangalia akivipitisha vidole vyake ndani ya nywele zake kana kwamba anapigana na hamu ya kuzing’oa. “Sasa shughulika na Trevor. Unaweza kunifanyia hilo? Mlete pamoja na Zakaria kwenye mkutano kesho.” Aliuuma mdomo wake wa chini asitake kusababisha fujo nyengine pale. “Na kwa sababu ya hiyo, sitachukua vitu vyangu usiku wa leo… ikiwa itakufanya uhisi vizuri.”

Chad aliitikia na akampa tabasamu dogo, “Sawa.”

Aliufungua mlango kutwatoa nje lakini wote walisita walipomuona Zakaria akiwa amesimama kati ya wanaume hao wawili kiganja chake kikiwaka moto akiwaelekea wote wawili.

“Jamani, tunaondoka,” Envy alisema na kuharakisha nje ya mlango akiushika mkono wa Devon akiharakisha kuelekea kwenye gari la Devon.

Trevor alianza kufuata lakin Zakaria alimzuia, “simama hapo, mpenzi. Tunahitaji kukabiliana na kaka yake kwanza.”

“Wacha tuingie ndani na nitatengeneza kahawa,” Chad alijitolea, akifuatia na pumzi ya shukrani wakati Trevor alipogeuka kwa hasira na kutembea kuingia nyumbani mwake kama mtu aliyekuwa mwito. Aliitikia wakati Zakaria alipomfuata Trevor ndani, kisha akaufunga mlango akijiuliza alijiingiza kwenye jambo gani.

Mara tu chombo cha kutengenezea kahawa kilipokuwa kikifanya kazi, Chad aliwageukia wageni wake wawili. Kwa wakati huo, alikuwa na maswali mengi kuliko majibu na hilo lilikuwa halisaidii chochote. “Sasa hili ni lipi analolisema Envy kuwa kuna pepo aliye huru? Pia alisema kuwa Warren anamuita kila mmoja kesho kwa mkutano aina fulani kuhusu kilicho fanyika usiku wa leo na anatutaka sisi watatu tuuhudhurie.”

Trevor hangejizuia kutoa tabasamu ndogo kucheza kwenye midomo yake. Kwa hiyo Envy alimtaka ahusike… alitaka kumueka karibu. Hange mlaumu. Jinsi alivyokuwa Devon akiimlinda, hange hisi kuwa salama sana. Akijua kuwa alimhitaji kuliifanya hasira yake kupotea.

“Tunge uvamia mkutano huo hata hivyo.” Alimuangalia Zakaria aliye thibitisha habari hiyo. Alitabasamu tena akitambua kuwa angemuona Envy baada ya saa kadha. Natumai ni wakati wa kukuambia kinacho endelea.”

Alijikunja kwa ndani jinsi alivyokuwa akiitumia nafasi yake kuwa karibu na Envy tena. Pia alijua jinsi itakavyoonekana kwa kila mmoja. Devon atafikiria kuwa alikuwa akimtumia Envy tena lakini hilo ndilo lililokuwa mbali sana na ukweli. Basi tena, hakuwa mbali na kumtumia kaka yake kuwa karibu naye na kufanya kazi yake kwa wakati huo huo. Itambidi Devon ajifunze kuwa kila kitu ni sawa kwa mapenzi na vita… na mbadili viungo bora ashinde.

“Niko masikio wazi,” Chad alinungúnika na kuiweka mikono yake kifuani ilikumfanya Trevor amuangalie kutoka mahali alipokuwa. Hakujifikiria kuwa mbashiri lakini alikuwa akifanya kazi nzuri ya kumsoma Trevor kwa wakati huo.

“Hatujui mengi kumhusu yule pepo, ila tu kwamba alikuwa amefungwa pale kwa karne kadha. Kuweko kwako kumeshinda chochote tulicho nacho katika faili zote pale P.I.T. lakini bado tunatafuta miongozo,” Zakariya alianza na kutumaini kuwa Trevor ataingilia.

“Kwa hiyo ulijua kuwa kulikuwa na pepo aliyefungwa kwa karne nyingi chini ya makaburi kwa muda usijua na hukufanya chochote kulihusu?” Chad alidai.

Trevor alimuinulia nyusi, “Unatarajia tufanye nini kulihusu? Tumsaidie kujifungua? Alikuwa amefungwa pale na hata hatukujua jinsi aliyeanguka na mfyonza damu walivyoweza kuivunja fingo ile iliyokuwa imemshikilia.”

“Aliyeanguka?” Chad aäliuliza. “Unamaanisha mmoja wa wale malaika Envy aliyeniambia kuwahusu?”

Zakaria aliitikia, “Ndio, tumejua kuwahusu kwa muda mrefu sana. Tunajua kuwa kuna wengine, lakini hatuwezi kuwaona mahali popote, na hata hao walioanguka wawili wanaoishi ndani ya mji hwakujua kuwepo kwa yule mwengine aliyefungwa kwenye kaburi hadi mmoja alipoenda hapo chini.”

“Pia tuna mmoja anayejua kukabiliana na mapepo,” Trevor alisema. “Tukiwa na bahati nzuri, ataweza kuifafanua tutakapo muita.”

“Hujachelewa sana kujitoa,” Zakaria alimwambia Chad. “Sema neno tu na tutafuta kila kitu kilichotokea kutoka kwenye kumbukumbu yako.”

Chad alikunja uso na akaanza kummiminia kila mmoja wao. Alikuwa polisi maisha yake yote kwa sababu alitaka kuleta utofauti. Lakini, zaidi ya mara moja, alihisi kana kwamba alikuwa hafanyi vya kutosha. Kila mara kulikuwa na muuza madawa ya kulevya, muuaji mmoja zaidi, mvunja sheria za barabarani mwengine… yote haikuonekana kutosha. Lakini kile ambacho Trevor na Zakaria walikuwa wakifanya kilileta utofauti… aina ya utofauti Chad alikuwa akitaka kufanya.

Akiinywa kahawa yake, alikiweka kikombe chake chini na kuitikia mara mora. “Niko ndani.”

*****

Anjelika aliamua kuwa simu zilikuwa mbaya kuliko mapepo wakati simu yake ilipoanza kulia saa tisa alfajiri. Alipoangalia aliyekuwa akimpigia, aliyakunja macho yake na kuishika. Aliiwasha na kisha kuzisukuma nywele zake ili aiweke dhidi ya sikio lake.

“Isipokuwa ulimwengu umepasuka, bahari zimegeuka nyekundu, tauni saba za Misri zimerudi, au unakufa, lazima kuwe na maelezo mazuri ya wewe kuniamsha,” alinguruma.

“Aw, njoo mpenzi… kwani unaongea hivyo na Zaki-dubu wako?”

Anjelika aliikata simu na kukiangusha kichwa chake tena kwenye mto. Alikuwa tu amerudi kulala wakati simu ilipolia tena. Bila ya kuiangalia simu, aliiwasha na kuongea tena.

“Nitakupata Zakaria,” alisema. “Wewe na mbwa wako mdogo pia.”

“Ole wangu, kumbukumbu za Mchawi wa Oz,” Zakaria alijifanya kushangaa, na Anjelika kwa siri alitabasamu kwa ajili ya mbinu za, na akafurahi kuwa hakuweza kumuona.

“Unataka nini?”, alikaa, akizisukuma nywele zake kutoka kwenye uso wake.

“Tumempata mmoja mbaya sana anayeitwa Mateso,” Zakaria alisema.

Anjelika alishuka pale kitandani na kuiwasha taa. “Mkubwa kiasi gani?”

“Sina uhakika, lakini na kisi kuwa ni wa kiwango cha saba.” Alitabasamu ndani ya simu akijua hili lingeupata umakini wake… na alipenda tu kuupata umakini wa Boo.

Anjelika aliingia sebuleni na kukiwasha kipakatalishi. Alipiga chapa mambo kadha kisha akaukunja uso.

“Kiwango cha saba? Unahakika?” aliuliza. Kitu chochote zaidi ya kiwango cha tano huwa hatari sana na nadra sana.

“Ni kisio tu,” Zakaria alijibu. “Kiliweza kumnasa mmoja kati ya wawili wa aina yetu ambaye tulikuwa tukimfuata na inaonekana kuwa aliyeanguka mwengine alikuwa pale chini naye kwa muda mrefu. Kwa sababu wanachukuliwa kuwa wa kiwango cha saba basi ninakisi kuwa chochote kilichokuwa na nguvu za kuweza kumfunga mmoja, yuko sawa naye.”

Anjelika alikuwa akiitafuta hifadhi data yake. Zaidi ya robo tatu ya data hiyo ilikuwa imepatikana kutoka kwenye hifadhi za Vatikani kinyume cha sheria, lakini hakuna aliye pingana na matokeo yake. Ukweli wa kwamba pepo wa kiwango cha saba huenda alikuwa amegunduliwa mjini Los Angeles ilikuwa sababu ya kutosha sio tu ya kumuamsha yeye, lakini wafanyakazi wote wa P.I.T pia.

Kila pepo aliwekwa kwenye daraja moja hadi kumi, kiwango cha kumi kikiwa sawa na Shetani mwenyewe. Alichukia kukumbana na yeyote aliyekuwa na uchawi kiasi cha kutosha kumfunga pepo wa kiwango cha saba… utahitaji ngurumo la Mungu kulitimiza hili.

“Sipati chochote kumhusu pepo anayeitwa Mateso kwenye eneo la Los Angeles,” alisema baada ya dakika chache. “Wacha niunganishe diski yangu ya nje kisha niziangalie hizo faili.”

Alimsikia Zakaria akiongea na mtu mwengine na akadhani kuwa alikuwa Trevor hadi alipoisikia sauti nyengine.

“Unaongea na nani?” aliuliza.

“Mwanachama mpya wa kundi letu, Chad,” Zakaria alijibu. “Ni afisa wa polisi anayejua mengi sana, kwa hiyo tulimleta ndani ili kuulinda umma, na kusema nina maanisha wale wapumbavu wengine anaofanya kazi nao.”

Anjelika alitabasama, “Huenda kukawa na wabaya zaidi huko nje.”

“Sio kwa pakubwa,” Zakaria alisema.

“Sawa,” Anjelika alisema. “Nimeisha iunganisha, wacha tuangalie yote niliyo nayo hapa.”

“Unamaanisha kuwa hujui?” Zakaria aliuliza kwa mshangao.

Anjelika alishusha pumzi, “unajua nilivyo. Ninge kisahau kichwa changu ikiwa hakingekuwa kimeshikiliwa. Nimepata fursa ya kuangalia tu sehemu ya kitu hiki.”

“Ndio uliipakua kwa haraka kubwa.” Zakaria alisema na kisha kushusha pumzi yeye mwenyewe. “wakati mzuri, wakati mzuri.”

Anjelika aliifungua diski na kuchapa neno ili kutafuta maana na kisha akabonyeza ingia.

“Kwa hiyo unamaanisha kuwa hujakuwa na tabia nzuri.” Anjelika aliuliza akiegemea nyuma ya kiti chake wakati tarakilishi ikifanya kazi yake.

“Hapana,” Zakaria alicheka. “Huwezi kunipeleka popote, kumbuka?”

Anjelika alikunja uso akikumbuka jinsi miezi miwili tu uliyopita wakati walipokuwa wameenda kwenye sherehe kubwa wakati wakimfukuza mbwa mwitu aliyekuwa na miaka minne aliyekuwa amepotea na hakulifurahia hilo. Ilipofika mwisho wa usiku huo, Zakaria alikuwa ameipoteza suruali yake kwa sababu yle mbwa mwitu alijibadili wakati alipokuwa katika hali ya hasira ya kitoto na kuirarua vipande vipande.

Sehemu ya kuchekesha zaidi ilikuwa kwamba Zakaria hakusema kitu chochote, aliivua tu na kutembea na suruali ya ndani na koti na suruali. Anjelika naye hakujua afanye lipi, kuona haya au kucheka. Kuiona miguu yake iliyokuwa na soksi zilizokuwa hadi magotini na viatu karibu kumuue wakati wasichana kadha walipomzunguka wakitaka kucheza densi naye.

Tarakalishi yake ilitoa mlio na akasongea mbele kuangalia kilichotokea katiak kutafuta kwake.

“Umepata chochote?” Zakaria aliuliza.

Anjelika alizifungua faili chache ambazo zilikuwa na neno Mateso ndani yao na akaanza kusoma. Sigara yake ilitoka mkononi mwake aliposoma na kusimama miguuni mwake.

“Ouch,!” alilaani na kuichukua sigara yake tena na kuizima kwa haraka.

“Kila kitu kiko sawa?” Zackaria alikunja uso kwa wasiwasi na kuuinua mkono wake juu wakati Trevor alipotaka kujua kilichokuwa kikiendelea.

Anjelika alizisoma habari tena ilikuhakikisha. “Ninachukua ndege ifuatayo kutoka hapa,” alimueleza kabla ya kuitoa simu kutoka sikioni mwake. Alilikatiza swali la Zakaria na kukiangalia tena kiwambo. Hakikuwa alichokisoma ndicho kilichomhakikishia kuwa hiki kilikuwa hatari… ilikuwa kwamba mkuu wa PIT alimnyima ruhusa ya kuifungua faili hiyo.

Ikiwa Storm alikuwa akiziweka siri… basi alitaka kujua ni kwa nini.

You've Just Finished your Free Sample

Enjoyed the preview?

Buy: http://www.ebooks2go.com